Mpendwa Mzazi/Mlezi,

Mwaka huu, mwanafunzi wako atakuwa akitumia Lexia® English Language Development,™ mpango wa masomo ulioboreshwa kutumia tarakilishi ambao umeundwa ili kusaidia Emergent Bilinguals katika gredi za K-6. Shughuli katika Lexia English husaidia uuaji wa lugha ya Kiingereza ya wanafunzi kupitia mazungumzo ya elimu na maudhui katika Hisabati, Sayansi, Elimujamii, Wasifu na Maarifa ya Jumla. Zimeundwa ili kuwasaidia wanafunzi wa Emergent Bilingual kujenga ufasaha wa lugha ya Kiingereza katika sehemu tatu muhimu: **kuongea**, **kusikiliza**, na **sarufi**.

Hii hapa namna ambavyo Lexia English hufanya kazi:

- Mwanafunzi wako anaanza mwanzo unaofaa mahitaji yake na anafanya kazi katika shughuli za mtandaoni wiki nzima.
- Shughuli za mtandaoni ni pamoja na mafunzo ya moja kwa moja, marudio na maoni mwanafunzi wako anapoendelea kupata stadi mpya.
- Maendeleo na utendaji katika mpango yanaripotiwa, kuruhusu walimu kutoa usaidizi unapohitajika.
- Vipindi vya ana kwa ana katika kuongea na kusikiliza pia hutumiwa kuimarisha na kujifunza stadi alizojifunza katika mpango wa mtandaoni.
- Vyeti va mafanikio vinaweza kutumwa nyumbani ili kusherehekea ufanisi na kuonyesha maendeleo ya mwanafunzi wako katika mpango.

Tunatumai utatangaza furaha yetu kuhusu mpango huu!

Wako mwaminifu,

______________________________________

## Lexia English inaweza kutumiwa nyumbani kwa zoezi la ziada. Kuanza ni rahisi!

1. Ili kutumia kwenye kompyuta, nenda kwenye https://english.lexialearning.com.
2. Ili kutumia kwenye iPad, pakua **Lexia English** app ya bila malipo kutoka kwenye App Store.
3. Mara ya kwanza mwanafunzi wako anapotumia Lexia English, huenda ukahitajika kuandika barua pepe ya mwalimu iliyoonyeshwa hapa chini. Kisha mwanafunzi wako anaweza kuingia akitumia jina la mtumiaji na nenosiri vilivyotumiwa kwenye shule na kuorodheshwa hapa chini.

| | |
|---|---|
| **Barua pepe ya Mwalimu** (kwa ajili ya mipangilio) | |
| **Jina la Mtumiaji** | |
| **Nenosiri** | |

Kwa maelezo zaidi kuhusu vifaa vya usaidizi au mahitaji ya ufundi, tembelea ukurasa wa Lexia's Support for Families kwenye Lexia Help Center. Maswali ya kiufundi pia yanaweza kuelekezwa kwa Lexia Support Team.

**Tafadhali fahamu kwamba Lexia Customer Support imeshindwa kutoa majina ya watumiaji au manenosiri ya wanafunzi, au barua pepe za walimu.**

# Kufikia Lexia® English Kutoka Nyumbani

Ni muhimu mwanafunzi wako afanye kazi bila usaidizi wowote anapotumia Lexia English. Kazi zote ambazo mwanafunzi wako anafanyia nyumbani zinarekodiwa na kuripotiwa kwa mwalimu. Kwa kufanya hivi, walimu wanaweza kuona wakati usaidizi unahitajika na kutoa maelekezo na msaada lengwa.

Ikiwa una swali kuhusu jina la mtumiaji au nenosiri la mwanafunzi wako, tafadhali wasiliana na mwalimu wa mwanafunzi wako.

## Kipakatalishi/Daftari/Tarakilishi

**1.** Fungua dirisha la kivinjari
*(Chrome tu ndicho kivinjari kinachokubalika).*

**2.** Nenda kwenye https://english.lexialearning.com

**3.** Ukidokezwa, andika barua pepe ya mwalimu ili uweke mipangilio ya kifaa.




**4.** Andika jina la mtumiaji na nenosiri la mwanafunzi.




**5.** Bofya kitufe chaLog*Log In*.

## iPad (iPad 4 au juu zaidi)

**1.** Tafuta **Lexia English** katika App Store.



**2.** Gusa kitufe cha ***Pakua/Sakinisha*** ili upakue Lexia English kwenye kifaa.

**3.** Pindi tu inaposakinishwa, gusa programu kwenye kifaa chako.

**4.** Ukidokezwa, andika barua pepe ya mwalimu ili uweke mipangilio ya kifaa.




**5.** Andika jina la mtumiaji na nenosiri la mwanafunzi.




**6.** Bofya kitufe chaLog*Log In*.

***Baada ya kuingia kwenye mpango, wanafunzi wataombwa warekebishe maikrofoni yao kwa kubofya maikrofoni na kuhesabu. Wanafunzi wanapofaulu kufanya hivyo, watasonga kwenye skrini yao ya Mwanzo.***

©2022 Lexia Learning, a Cambium Learning® Group company. All rights reserved. Lexia grants permission to reproduce this letter.

LE-HOMELTR-ACC-SW-0822